# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO**

***KOROGWE* DVTC 2025**

**Simu: 0754855742** **P.O Box 641 *KOROGWE***

**Nukushi:0769914505** **Baruapepe: korogwedvtc@veta.go.tz**

13/01/ 2025

**Kumb. Na:**

**Ndugu: ..................................................**

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA KOROGWE DVTC MWAKA 2025**

**MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MAZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI**

1. Uongozi wa chuo cha Korogwe DVTC unachukua nafasi hii kukupongeza, na kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na Chuo tajwa hapo juu katika Fani ya...................................................................,
Ngazi ya kwanza (level one), Kutwa/Bweni

2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili - mitatu (2-3)
3. Chuo kimefunguliwa rasmi kwa mafunzo tarehe 13 Januari, 2025
   JIANDAE VEMA NA URIPOTI CHUONI MARAMOJA.
4. Unatakiwa kuthibitishwa na Daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyochagua.
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyochagua.
6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa na barua hii.
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo/kusajiliwa.
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni
9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama inavyoelekezwa na barua hii.
10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. Unashauriwa Fedha ikishalipwa hairudishwi.

11. **Kuripoti Chuoni.** Nafasi yako itafutwa Utakaposhindwa kuripoti katika muda wa wiki mbili baada ya Chuo Kufunguliwa.

.................................

**JOYCE I. MAKYAO**
**MKUU WA CHUO**

12. **Mwanzo wa Muhula 2025.** Mafunzo yataanza Jumatatu tarehe **13 Januari, 2025**. Nafasi yako atapewa Mtanzania mwingine ukishindwa kufika Chuoni hadi **18 Januari 2025.**
13. **Muda wa Mafunzo.** Mafunzo yamepangiliwa kwa hatua tatu. Hatua ya Kwanza (Level I ), Hatua ya Pili (Level II) na Hatua ya Tatu na ya mwisho (Level III ).
14. **Sifa zako.** Unatakiwa kuja na cheti halisi cha kumaliza shule (original academic certificate/result slip) na nakala yake (photo copy). Baada ya cheti kuthibitishwa na Msajili/Dawati la Kujiandikisha, utaruhusiwa kuondoka na cheti chako halisi na nakala kubaki Chuoni kwa kumbukumbu.
15. **Usalama**. Unatakiwa kujinunulia Safety Boots yenye sifa zifuatazo:- steel toe cap; oil resistant sole. (*Wanafunzi wa Secretarial & Computer na Food Production /Dual Hotel hawahusiki*). Ikiwa huna uhakika na Maelekezo yoyote hapa, fika Chuoni Ofisi ya Msajili kwa Ufafanuzi.

16. **Mahitaji Maalum** Unatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako binafsi Ukiwa Chuoni. Kila mwanafunzi anaelekezwa kuzingatia na kutekeleza maelekezo haya hapa.
    a. Mashati mawili meupe (mikono mifupi) ya tetroni. (Nembo Utapewa Chuoni)
    b. Suruali 2pc rangi ya Bluu nyeusi – zingatia vipimo ulivyopewa (Upana wa chini Inch 15 au Cm 38 na zenye linda)
    c. Jozi moja ya viatu vyeusi vya Ngozi na Safety boot kwa ajili ya karakana kwa fani za uhandisi.
    d. Vifaa vya hesabu (mathematical set) Kalamu na penseli
    e. Daftari 10 aina ya counter book 4 quire.
    f. Mavazi ya heshima (No Crazy dress/jeans na mavazi ya hovyo/raruraru Hayaruhusiwi na vifaa vya usafi binafsi.
    g. Ovaroli – rangi ya blue kwa fani za uhandisi
    h. Kitambulisho cha Bima ya afya NHIF
    i. Photocopy paper ream 1
    j. Fyekeo1, jembe1, reki1,Panga 1 na fagio la chelewa lenye mshikio
    **WANAFUNZI WA BWENI**
    k. Shuka mbili za rangi ya bluu bahari kwa wavulana na Pink kwa wasichana
    l. Mto wa kulalia.

17. **SHERIA ZA CHUO.** Chuo cha VETA *KOROGWE* DVTC kinazo Sheria na Kanuni kwa Mujibu na Muongozo Uliotolewa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania (VETA) Nakala imeambatanishwa na barua hii..
18. **Ada.** Ada ya Mafunzo kwa Mwaka Imeambatana na gharama ya mahitaji yaliyo-orodheshwa kwenye jedwali hapa chini. Yote yanalipwa Pamoja. Tafadhali zingatia maelekezo unayopewa katika ulipaji wa ada yako.

**JEDWALI LA MALIPO YA ADA NA GHARAMA NYINGINE 2024**

| MWAKA WA KWANZA 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **ADA** | **KUTWA** | **BWENI** | **MAELEKEZO** |
| ADA YA MAFUNZO | **60,000.00** | **120,000.00** | **PATA CONTROL NUMBER** |
| **MICHANGO MINGINE** | | | |
| NEMBO YA VETA 2PC | 5,000.00 | 5,000.00 | **LIPA KWENYE CONTROL NUMBER UTAKAYOPEWA CHUONI** |
| TAHADHARI | 20,000.00 | 20,000.00 | |
| KITAMBULISHO | 5,000.00 | 5,000.00 | |
| MICHEZO | 10,000.00 | 10,000.00 | |
| PICHA YA KITAMBULISHO | 1,000.00 | 1,000.00 | |
| FULANA YA CHUO | 15,000.00 | 15,000.00 | |
| **JUMLA MICHANGO MINGINE** | **116,000.00** | **176,000.00** | |
| **BIMA YA AFYA YA NHIF** | | | |
| **BIMA YA AFYA** | 50,400.00 | **50,400.00** | **LIPA KWENYE CONTROL NUMBER UTAKAYOPEWA YA NHIF UFIKAPO CHUONI** |

19. <u>**UTARATIBU WA MALIPO**</u>
    **Mwanafunzi afike Chuoni VETA *KOROGWE* atapewa namba ya malipo kwa serikali (control number) ya kulipia ADA** na michango mingine.
20. **ADA ZA MTIHANI.** Watakaofanya vizuri katika mafunzo na kufikia viwango/sifa za ufaulu, wataruhusiwa kufanya Mtihani wa Taifa "Competence Based Assessment" [CBA] na watapaswa kulipia ada ya mtihani huo. Wazazi/Walezi watataarifiwa Kiasi cha ada wakati wa likizo ndefu, mwezi Juni/Julai 2025.
21. **BIMA YA AFYA.** Kila Mwanafunzi Anatakiwa kuwa na Bima ya Afya NHIF. Endapo unayo Bima ya nyumbani uje nayo La sivyo uje na malipo yake kama inavyoonyeshwa hapo juu.
22. **KUPOKELEWA.** Waliolipa ada kamili, Kuwa na vifaa vilivyotajwa na kutimiza masharti yote yaliyoandikwa hapo juu, <u>Ndio Watapokelewa Chuoni</u>. Utatakiwa kuonyesha vitu hivi Kwa Mwalimu Dawati la kusajiliwa Chuoni Utakaporipoti na Utapewa Kibali cha Usajili Ili kupokelewa katika Fani yako.

***Nakutakia Mafunzo Mema Na Karibu Sana VETA - KOROGWE.***

## VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

**To Medical Officer (Government Hospital)**

………………..........................………..……………

……………………………….............................……

……………………………..................................………..

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine the above named candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as………………………………………………………………………………………

i) Eye sight…………………………………………………………………………….........

ii) Hearing …………………………………………………………………………….........…

iii) Asthma…………………………………………………………………………….........….

iv) Other serious disease……………………………………………………….............

**MEDICAL CERTIFICATE**:

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Date……………Designation…………………………..Signature & Official stamp…………………………

## KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**a) MWANACHUO**

Mimi …………………………………………………ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa na nina ahidi kuzingatia sheria na kanuni za Chuo.

Sahihi………………………………………………Tarehe………………………………………………………………

**b) MDHAMINI:**

Mimi………………………………………………..S.L.P.……………………Wilaya/Mkoa………………………………..
Ninathibitisha kuwa ninamdhamini aliyetajwa hapo juu na nitamlipia ghrarama zote za mafunzo (ada) n.k. pamoja na nauli wakati wote wa kwenda Chuoni na kurudi nyumbani kwa likizo na baada mafunzo.

Tarehe…………………………………Sahihi…………………………………………….

Nambari za Simu ………………………………………………………………………………

## SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI

**ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:**

### 1. MAHUDHURIO:

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1.20 asubuhi. Hii inamaana ifikapo saa 1.30 wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni. **Adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji**.

(b) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya Chuo kwenda nyumbani, Hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na mwalimu (mkuu wa sehemu) kwa kujaza fomu maalum.

(c) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari zifike chuoni, kwa ajili ya kumbukumbu na kukiwezesha chuo kuchukua hatua.

(d) Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi hataruhusiwa kufanya mitihani ya kumaliza masomo/mafunzo hivyo, hatapata cheti cha kuhitimu mafunzo.

### 2. MAVAZI

(a) Sare ya Chuo ni suruali ya Blue na shati jeupe la mikono mifupi. Sare hiyo itavaliwa wakati wote na iwe imechomekewa na shati ziwe safi, aidha sare hiyo itavaliwa wakati mwanafunzi atokapo nje ya chuo kwa ajili ya utambulisho.

(b) Vazi la ovaroli/aproni litavaliwa tu wakati wa vipindi vya kazi za mikono.

(c) Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu. Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au sandosi (sandles) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.

(d) Fulana maalum za chuo zitavaliwa siku ya Jumatano na Ijumaa tu. Pia wakati mwanafunzi atokapo nje ya chuo kwa ajili ya utambulisho.

### 3. USAFI WA MWILI

(a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote ile wakati wa masomo.

(b) Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato wakati wa masomo.

(c) **NYWELE KWA WAVULANA**:

(i) Zikatwe ziwe fupi na mtindo kama PANKY, AMERICAN BASE na KIPARA haviruhusiwi kabisa.

(ii) Hairuhusiwi kufuga ndevu.

(d) **NYWELE KWA WASICHANA**:
Nywele zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari (Utii wa Rhoda)

**NB**: Nywele ndefu na nywele zenye kupakwa madawa kama vile curl, raster na golden hair haziruhusiwi kabisa kwa kipindi chote cha mafunzo.

**4. WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:**

(a) Vitendo vyote vya wizi havirusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au mali ya mwanafunzi mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja na kukabidhiwa kwa vyombo vya dola.

(b) Ukipoteza vifaa vya chuo utatakiwa kulipa sawia, baada ya gharama hizo kufanyiwa tathimini na Afisa ugavi wa chuo.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinacho fanana na vile vilivyoko ndani ya chuo. Kama atakuja nacho akiandikishe getini na kwa mwalimu husika. Kinyume cha hapo kitatambuliwa kama mali ya chuo.

(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na wakati wa kutoka getini.

**5. UGOMVI**

Lugha chafu, lugha za mitaani, matusi, kupigana au kushambulia ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na vitendo ya namna hiyo atafukuzwa chuo mara moja; aidha kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola kwa hatua nyingine.

**6. ULEVI:**

Ulevi, uvutaji wa bangi, sigara, mirungi, ugoro, utumiaji wa madawa ya kulevya haviruhusiwi. Iwapo itabainika kwamba mwanafunzi analewa, au kuonekana katika sehemu za vileo anavuta sigara, anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa chuo mara moja.

**7. MAPENZI**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hauruhusiwi kabisa.

(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bila ya kibali au ruhusa.

**8. MIGOMO**

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusabibisha migomo atafukuzwa chuoni mara moja.

9. **LUGHA**
Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingireza.

10. Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa udhibitisho na ajulishwe Mkuu wa chuo mara moja.

11. Wakati wa masomo mwanachuo haruhusiwi:

(a) Kuendesha baiskeli sehemu za madarasa na karakana ukipatikana na hatia adhabu kali itatolewa.

(b) Vyombo vyote vya usafiri (baiskeli na pikipiki) zitaegeshwa sehemu moja. Kila mmoja anapaswa kufunga chombo chake cha usafiri kwa ajili ya usalama.

(c) Kwa namna yoyote hairuhusiwi kutumia simu, ikibainika utanyang'anywa mpaka siku ya kufunga chuo.

## ONGEZEKO LA SHERIA KWA WANACHUO WA BWENI

12. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo tu:-
(i) Jumapili tangu saa 12 asubuhi hadi saa 11:30 jioni.
(ii) Jumamosi tangu saa 7:30 mchana hadi saa 11:30 jioni.
(iii) Siku nyinginezo za mapumziko zinazotambulika kitaifa kuanzia saa 3 asubuhi hadi saa 11:30 jioni.
(iv) Waislamu wataruhusiwa kwenda msikitini siku ya Ijumaa saa 6:30 adhuhuri na kurudi baada ya ibada saa 7:30 mchana.
(v) Wasabato (SDA) wataruhusiwa kwenda kanisani siku ya Jumamosi saa 1:00 na kurudi baada ya ibada saa 7:00 mchana.

**Hairuhusiwi kutoka nje ya Chuo wakati mwingine wowote bila kibali maalum.**

13. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuvaa sare ya Chuo yenye nembo ya VETA. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kuvaa sare yenye nembo ya VETA atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini na iwapo atakosa sehemu ya kukaa atajifukuzisha chuo.

14. Mwanachuo atakayethibitika na kosa la kulala nje ya chuo bila ruhusa atasimamishwa masomo mara moja.

15. Hairuhusiwi kupika chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.

16. (a) Ni marufuku wanachuo wa kiume na wakike kutembeleana mabwenini.
(b) Hairuhusiwi **KABISA** kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa chuo bila ruhusa au kibali.

17. Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu au mwalimu mlezi wa bweni itatolewa.

18. (a) Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4.00 za usiku. Ikibainika hatua kali zitachukuliwa ikiwemo ya kunyang'anywa nafasi ya bweni.

(b) Wanachuo wa bweni hawaruhusiwi kuonekana sehemu ya bweni wakati wa masomo bila ya ruhusa ikubaiinika adhabu kali itatolewa.

19. (a) Hakuna ruhusa kumkaribisha wala kumlaza mgeni bwenini. Ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu maalumu ya mazungumzo.

- Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7.00 mchana hadi saa 10.30 jioni
- Kila Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 2.00 asubuhi mpaka 10.00 jioni.

(c) Wanafunzi wa kutwa hawaruhusiwi kwenda bwenini bila ruhusa ikibainika adhabu kali itatolewa.

20. Marufuku kuwa na vifaa vifuatavyo bwenini:

- Heater
- Jiko
- Music System
- Panga
- Kisu na vitu vingine vinavyofanana na hivyo. Vikikamatwa havitarudishwa na kupewa adhabu kali ikiwemo kunyang'anywa nafasi ya bweni.

21. (a) Vyumba/ Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.

(b) Marufuku kupita kwa kuruka kuta za wingo wa chuo. Hatua kali zitachukuliwa ikiwemo kusimamishwa masomo.

22. Ruhusa ya kulala nje ya mipaka ya chuo itatolewa na ofisi ya Mkuu wa Chuo baada ya mhusika kujaza fomu na kuruhusiwa.

23. Kila mwanafunzi atakayetoka nje ya chuo ataandika jina kamili, namba ya kitambulisho katika kitabu cha kutoka, aidha wakati wa kurudi ataweka sahihi na muda kamili kukamilisha ruhusa hiyo.